# JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
## OFISI YA RAIS – TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA
## HALMASHAURI YA WILAYA LUSHOTO
## SHULE YA SEKONDARI SHAMBALAI

**Mawasiliano:**

Mkuu wa Shule: 0784 787 915

Makamu M/Shule: 0713 592 981

Patron: 0764 609 956

Kumb.Na: **SSS/C/PS/V.1/2023/1**

Kwa ..............................................................
..............................................................

## FOMU YA MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA KIDATO CHA TANO MWAKA 2023/2024 KATIKA SHULE YA SEKONDARI SHAMBALAI

### SEHEMU A: UTANGULIZI

1. Ninayo furaha kukupongeza kwa kuchaguliwa kwako kihalali kujiunga na Shule hii katika kidato cha TANO 2023/2024. **KARIBU SANA** Shule ya Sekondari Shambalai. Ni shule ya Bweni kwa kidato cha tano na sita kwa Wavulana. Aidha, ni shule yenye Tahasusi za Masomo ya Sanaa ("Subject Combinations") HGL & HKL Nina imani kwamba utafurahi/utafaidika kusoma katika shule hii.
2. Ukiwa shule ya Sekondari Shambalai, utalazimika kufuata Sheria, Kanuni, Taratibu za Shule kama zilivyoanishwa katika fomu hii ya kujiunga na kidato cha tano.
3. Shule itafunguliwa siku ya Jumamosi tarehe **13/08/2023** kwa ajili ya kuanza masomo siku ya Jumatatu tarehe **31/08/2023**.
4. Shule iko katika Halmashauri ya Wilaya ya Lushoto mkabala na Hospitali ya Wilaya ya Lushoto. Pia ipo umbali wa Kilometa 2 kutoka kituo cha mabasi Lushoto mjini. Usafiri wa kutoka kituo cha mabasi hadi shuleni ni gari ndogo maarufu VIDOCHI nauli ni shilingi 500/= au usafiri wa pikipiki (bodaboda) ni shilingi 1,000/= Ama kwa wale wanaotoka nje ya wilaya ya Lushoto au mikoani shuka kwa **msabaha** au **hospitali ya wilaya** kisha uliza ilipo shule ya Sekondari Shambalai utaoneshwa utatembea pasipo kutumia usafiri.

### SEHEMU B: SARE ZA SHULE

Mwanao aje na:-

i. Suruali mbili (2) rangi Nyeusi (Zitatumika Darasani)
ii. Suruali mbili (2) rangi Nyeusi (zitatumika kama Shamba dress)
iii. Shati Nyeupe Jozi mbili (2) mikono mirefu.
iv. Fulana mbili (2) rangi nyeusi (Shingo ya duara) zisiwe na picha wala maandishi yeyote, iwe ya mikono mifupi (zitatumika kama Shamba dress)
v. T-shirt rasmi ya Shule inapatikana Shuleni Tshs. 12,000/= uje nayo mkononi.
vi. Shuka Mbili Rangi ya bluu bahari na Blanket 1
vii. Jacket jeusi, kwa ajili ya kujikinga na baridi lisiwe na kofia wala maandishi.

viii. Viatu vyeusi vya ngozi, siyo buti na visiwe na visigino virefu.
ix. Soksi rangi nyeupe.
x. Mkanda mweusi wenye kifugio cha Kawaida
xi. Sweta rangi ya bluu yenye V-shape shingoni, linapatikana shuleni 15,000/= aje nayo mkononi.
xii. Nguo za michezo pamoja na raba kwa ajili ya kukimbia mchakamchaka

**SEHEMU C: UJE NA VIFAA VIFUATAVYO:**

i. Jembe lenye mpini 1, panga1, Ufagio wa chelewa 1, squeezer 1.
ii. Ndoo mbili ndogo za plastiki zilizo safi
iii. Vyombo vya vyakula ambavyo ni sahani, kijiko na kikombe
iv. Sanduku la bati size ya kati. Masanduku mengine hayaruhusiwi.
v. Begi la Darasani [School bag] na Mathematical set kwa tahasusi ya HGL.
vi. Daftari zisizopungua Nane (08) counterbook
vii. Karatasi kwa ajili ya mitihani Rimu 2 aina ya A4 atatoa kwa kila mwaka
viii. Nakala ya Cheti cha Kuzaliwa.
ix. Result slip ya Kidato cha Nne nakala itabaki kweye file. (Hautapokelewa kama huna Resut Slip)
x. Uje na godoro la futi mbili na nusu
**xi. Hakikisha kuwa Mwanafunzi ajapo Shuleni awe na Bima ya Afya**

**SEHEMU D: MICHANGO MINGINE**

(LIPA KWENYE AKAUNTI YA NMB NAMBA **41601100002** YENYE JINA LA **SHAMBALAI SECONDARY SCHOOL**)

| Na | Aina ya Mchango | Kiasi |
|---|---|---|
| 1. | Mchango wa Uendeshaji wa Shule | 65,000/= |
| 3. | Tahadhari | 5,000/= |
| 4. | Nembo | 5,000/= |
| 5. | Kitambulisho cha Shule | 5,000/= |
| | **Jumla** | **80,000/=** |

**Viambatanisho Na Fomu Muhimu**

a. Fomu ya uchunguzi wa afya (medical examination form) ambayo itajazwa na Mganga mkuu wa hospitali ya serikali
b. Fomu ya maelezo binafsi kuhusu historia ya mwanafunzi au mkataba wa kutoshiriki katika mgomo, fujo na makosa ya jinai.

**KARIBU SANA SHULE YA SEKONDARI SHAMBALAI**

Godson C Mshana
**Mkuu wa Shule**
**0784787915**

MKUU WA SHULE
SHULE YA SEKONDARI SHAMBALAI
LUSHOTO

**SHULE YA SEKONDARI SHAMBALAI**
**HISTORIA YA MWANAFUNZI (Ijazwe na Mwanafunzi na Mzazi/Mlezi)**

1. Jina la mwanafunzi… …………………………………………………………………………(Jina liwe sahihi na CSEE)
Tarehe ya kuzaliwa..........................… Wilaya…………………......... Mkoa……..…………
(iii) Dini………………………. Dhehebu……………………………
(iv) Shule ulizosoma kabla ya kuja Sekondari ya Shambalai

| | JINA LILILOANDIKISHWA SHULENI | SHULE YA MSINGI/SEKONDARI | MWAKA ULIOMALIZA |
|---|---|---|---|
| 1 | | | |
| 2 | | | |

**Saini ya Mwanafuzi.................**

2. MAJINA YA WAZAZI
   a) **Baba:**
      Jina:............................................................... *Yupo hai/Amefariki
      Kazi:..............................................................
      Dini:............................................. Dhehebu:............................
      Anwani:.......................................................... Simu Namba:......................
   b) **Mama:**
      Jina:.............................................................. *Yupo hai/Amefariki
      Kazi:.............................................................
      Dini:............................................................ Dhehebu:............................
      Anwani:........................................................ Simu Namba:......................
3. Jina la atakayegharamia mahitaji ya shule
   Jina:....................................................................
   Uhusiano:...............................................................
   Namba ya Simu:....................................................

4. **Uthibitisho wa mwanafunzi**

Mimi…………………………………………………………………ninakiri kuzisoma na kuzielewa taratibu/sheria za Shule ya Sekondari Shambalai hivyo ninakubali kwa hiari yangu, kujiunga na shule ya Shambalai na kuthibitisha kuwa nitafuata Sheria na taratibu zote za shule hii, ili nitimize lengo kwa manufaa yangu/familia na taifa kwa ujumla. Endapo nitakuwa kinyume na sheria/taratibu za shule nitakubali kuadhibiwa. Naahidi kutokuchelewa kurudi shuleni baada ya likizo fupi na ndefu.

Saini ya mwanafunzi……………………………………………Tarehe……………………….

5. **Uthibitisho wa Mzazi/Mlezi**

Mimi…………………………………………………………………ninakiri kuzisoma na kuzielewa taratibu/sheria za Shule ya Sekondari Shambalai, hivyo ninathibitisha kuwa nitatoa gharama zote za shule pamoja na mahitaji mengine, kwa lengo la kumwezesha Mwanafunzi aliyetajwa hapo juu asome katika mazingira mazuri kwa kipindi chote atakachokuwa hapo shuleni, kwa kuzingatia sheria na taratibu za shule ya Sekondari Shambalai. Aidha nathibitisha kwamba yaliyoandikwa hapo juuni sahihi. Naahidi kwamba mtoto wangu hatachelewa shule kwa kukosa mahitaji (michango nk)

Saini ya Mzazi/Mlezi……………………………………Tarehe……………………………

*Kata isiyohusika.

The united Republic of Tanzania

**PO- Regional Administration and Local Government**

Shambalai Secondary School

P.O BOX 52 Lushoto

Ref.No. SSS/C/PS/V.1/12

To the Medical Officer

……………………………………,

……………………………………..….,

…………………………………….

## REF: A STUDENT'S MEDICAL EXAMINATIONS FORM

Please, examine the Student……………………………………………………………… in respect of these areas and any other area(s) deemed fit Please. Delete whichever applies.

Does the Student have problems in connection with…….. ?

a) Sight Yes/No. If yes, state…………………………………………………………......

b) Hearing. Yes/No. If yes, state ……………………………………………………….…..

c) T.B or any other Chronic Diseases. Yes/No. If yes, state……………...............................

d) Blood Pressure. Yes/No. If yes, state…….......……………………….……………………

e) Any Physical Impairment(s).Yes/No. If yes, state ………………………….………………

Do you therefore recommend this pupil to pursue studies at this school?

……………………………………………………………………………………………..

Name……………………………………..Signature……………………..Date…………..…

Official Title…………………………………… Official Stamp.

# HALMASHAURI YA WILAYA YA LUSHOTO
# SHULE YA SEKONDARI SHAMBALAI
## SHERIA NA KANUNI MUHIMU ZA SHULE

1. **UVAAJI WA SARE NI LAZIMA KWA WANAFUNZI WOTE WAKATI WA:-**
   **1.1.** Masomo darasani
   **1.2.** Wanafunzi wanapotoka nje ya shule
   **1.3.** Mhadhara wa Shule (BARAZA)
   **1.4.** Maandamano ya kitaaluma
   **1.5.** Mikutano
   **1.6.** Mahafali ("Graduation")
   Mwanafunzi atatakiwa kuvaa **shamba dress** awapo katika eneo la shule nje ya muda wa vipindi vya kufundishwa Darasani na **SI VINGINEVYO.**

2. **SEHEMU AMBAZO MWANAFUNZI HARUHUSIWI KUONEKANA**

Ni marufuku kuonekana sehemu zifuatazo:-

2.1 Vilabu vya pombe (Bars, Night Clubs,)
2.2 Majumba ya Starehe (Cinema Halls, Disco Halls nk)
2.3 Majumba ya kufikia wageni (Guest Houses)

3. **SHERIA NA KANUNI MUHIMU ZA SHULE:**

Shule inaendeshwa kwa mujibu wa Sheria ya Elimu Na. 25 ya mwaka 1978 na kama ilivyo rekebishwa kwa Sheria Na. 10 ya mwaka 1995. Aidha, inazingatia miongozo yote inayotolewa na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia yenye dhamana ya elimu na Ofisi ya Rais – TAMISEMI yenye jukumu la usimamizi na uendeshaji wa elimu nchini. Unatakiwa kuzingatia mambo ya msingi yafuatayo ambayo yanafafanuliwa kwa maandishi na utapewa nakala yake mara baada ya kuripoti shuleni. Mambo hayo ni pamoja na

i. Heshima kwa viongozi, wazazi, wafanyakazi wote, wanafunzi wengine na jamii kwa ujumla, ni jambo la lazima.
ii. Mahudhurio mazuri katika kila shughuli ndani na nje ya darasa ni muhimu.
iii. Kutimiza kwa makini maandalio ya jioni (Preparation).
iv. Kuwahi katika kila shughuli za shule na nyingine utakazopewa.
v. Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifu maelekezo juu ya kuwepo ndani na nje ya mipaka hiyo wakati wote wa uanafunzi wako katika shule hii.
vi. Kutunza usafi wa mwili na mazingira ya shule.
vii. Kuvaa sare ya shule wakati wote unapotakiwa kufanya hivyo.
viii. Kuzingatia ratiba ya shule wakati wote.
ix. Kuzingatia usafi (usitupe taka/ karatasi au uchafu ovyo)
x. Ni marufuku mwanafunzi kumiliki vifaa vyenye ncha kali na dawa bila idhini ya daktari; na
xi. Mwanafunzi haruhusiwi kubadili dini wala kumshawishi mwanafunzi mwenzake kubadili dini wawapo shuleni.

**MUHIMU:**

- **Mwanafunzi hapaswi kuja na simu shuleni kwa namna yoyote ile, na hakuna mtumishi anayeruhusiwa kutunza simu ya mwanafunzi;**

- **Mwanafunzi awapo shuleni atatakiwa kulala kwenye Bweni alilopangiwa na kitanda alichopangiwa. Ni marufuku mwanafunzi kulala kitanda kimoja na mwenzake au kuishi kwenye Bweni ambalo hakupangiwa. Kitanda kimoja kitatumika na mwanafunzi mmoja tu;**
- **Mwanafunzi ataruhusiwa kurudi nyumbani kwa ruhusa na kibali maalum toka kwa Mkuu wa Shule. (Msiba au Ugonjwa**).

4. **MAKOSA YANAYOSABABISHA MWANAFUNZI KUFUKUZWA SHULE**

**a)** Wizi,
**b)** Uasherati/ubakaji/ulawiti/ushoga,
**c)** Ulevi wa aina yoyote
**d)** Uvutaji wa sigara/bangi/utumiaji wa dawa za kulevya,
**e)** Makosa ya jinai,Kupigana au kupiga,
**f)** Kuharibu mali ya mtu/ umma/fedha ya serikali kwa makusudi.
**g)** Kuandika maandishi na michoro kwenye kuta za shule, milango n.k ni marufuku.
**h)** Kudharau bendera ya taifa/viongozi wa serikali, misafara ya viongozi wa kitaifa
**i)** Kuoa au kuolewa,
**j)** Kupata mimba/kumpa mwanamke mimba,
**k)** Kushiriki matendo ya uhalifu, siasa na matendo yoyote yale yanayovunja sheria za nchi,
**l)** Kutembelea majumba ya starehe na nyumba za kulala wageni,
**m)** Kulala nje ya shule bila kibali cha mkuu wa shule,
**n)** Kutoa mimba/kushiriki katika kutoa mimba,
**o)** Kutohudhuria vipindi vya darasani kwa muda mrefu bila taarifa/utoro,
**p)** Kutoa lugha chafu kwa wanafunzi wenzake,walimu/walezi na jamii kwa ujumla,
**q)** Kufuga ndevu, mustachi au nywele ndefu pamoja kucha.,
**r)** Kujipamba kwa kwa hereni, poda, kupaka kucha rangi,
**s)** Kugoma, kuchochea au kuongoza au kuvuruga amani na usalama wa shule au watu,
**t)** Kufanya jaribio lolote la kujiua, au kutishia kujiua kama kunywa sumu n.k.,
**u)** Kukataa adhabu kwa makusudi,
**v)** Kutoka nje ya shule bila sare ya shule au bila kibali,
**w)** Kumiliki, kukutwa au kutumia simu ya mkononi/line ya simu/charger/Flash/memory card katika mazingira ya shule. Kosa hili linaambatana na kulipia uharibifu wa miundombinu ya umeme kiasi cha shilingi laki moja taslimu,
**x)** Kutumia vyombo vya umeme Bwenini/ darasani au mahali popote ndani ya Shule.

**MUHIMU KWA MZAZI**

**a)** Mchango **WOWOTE** utakaotakiwa na shule ni lazima uwe na maandishi pamoja na Saini na muhuri wa Mkuu wa Shule. Kinyume cha hapo usimpe mwanao mchango ambao hauna barua.
**b)** Mpatie mwanao kitabu kigodo cha DINI kulingana na imani yako mfano BIBLIA au QURAN ili aweze kujifunza maneno ya Mungu awapo shuleni.
**c)** BIMA YA AFYA KWA KIJANA WAKO NI LAZIMA. Hakikisha akija Shuleni awe na Bima ya Afya.

# HALMASHAURI YA WILAYA YA LUSHOTO
# SHULE YA SEKONDARI SHAMBALAI
# ORODHA YA VITABU A-LEVEL.

| S/N | SOMO | VITABU |
|---|---|---|
| 01 | HISTORY | 1. Essentials in Advanced history paper I \|& II (Salehe Yasini).<br>2. Themes in Advanced History paper I & II (Florence M.Mavunde).<br>3. Advanced Level History Paper I & II (Zisti Kamili)<br>4. Contemporary Historical Events Advanced Level History<br>Shibitali & Son publishers ( Tumaini S.CK 2010) |
| 02 | GEOGRAPHY | 1. A comprehensive Approach to Physical Geography (D.T. Msabila).<br>2. Elementary Physical Geography: Advanced level and Colleges ( Ahmed Lubwama).<br>3. Practical Geography: Map reading, Photography and Surveying (Zisti Kamili |
| 03 | KISWAHILI | 1 .Nadharia ya Lugha ya Kiswahili kidato cha Tano na Sita (N. Nyangwine & Masebo)<br>2. Sarufi Maumbo ya Kiswahili Sanifu ( SAMAKISA) Sekondari na vyuo ( Kihore, Y.M. Masamba D.P.B, TUKI (2003)<br>3. Kamusi ya Kiswahili Sanifu, Toleo la pili: EnglishKiswahili Dictionary TUKI |
| 04 | ENGLISH LANGUAGE | 1. An Essential Guide paper I & II (Nicholus Asheli).<br>2. New Intergreted Advanced Level, Paper I & II (G.Mshana).<br>3. Grammar and Phonology Paper I (Michael Kadege).<br>4. Possibilities Questions and Answers Paper I & II (Mgonja. H)<br>5. Oxford Dictionary |
| 05 | GENERAL STUDIES | 1. General Studies for Advanced Level Certificate By Richard Mbalase (2011).<br>2. Understanding Advanced Level General Studies By Jonnes Bigirwamungu (2010).<br>3. Advanvced Level General Studies By Nyambari Nyangwine (2012). |